

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TAREHE 19 AGOSTI, 2020

Ndugu Wananchi wa Mkoa wa Rukwa, kwa muda wa zaidi ya Miaka Ishirini na Tatu (23), Mkoa wa Rukwa umekosa timu ya Mpira wa Miguu inayoshiriki Mashindano yenye Sura ya Kitaifa. Hali hii imekuwa na athari kubwa hususani ya maendeleo ya Soka katika Mkoa wetu wa Rukwa; sanjari na manufaa mengine ya Kiuchumi na Kijamii.

Kutokana na hali hiyo Mkoa kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali uliamua kuukarabati Uwanja wa Nelson Mandela na hatimaye Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF) kuamua Fainali ya Kombe la Shirikisho kati ya Simba Sports Club na Namungo FC kucheza katika Uwanja huo uliopo Mjini Sumbawanga.

Ndugu Wana – Rukwa, Ufanisi wa Fainali ya Kombe la Shirikisho (ASFC) ulikuwa chachu ya kutafuta timu ya Ligi Kuu ili kuleta furaha kwa Wananchi wa Rukwa na Mikoa jirani, kukuza Vipaji vya soka pamoja na kuinua hali ya Uchumi wa Wananchi wa Rukwa kwa ujumla.

Baada ya juhudi hizo kubwa kufanyika, napenda kuthibitisha taarifa kuwa Timu ya Tanzania Prisons imeamua kuhamia

Rukwa na kutumia Uwanja wa Nelson Mandela kama Uwanja wake wa Nyumbani katika Ligi Kuu kuanzia tarehe 16 Agosti, 2020.

Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru sana Kamishna Jenerali Seleman Mzee, Mkuu wa Jeshi la Magereza kwa kuridhia timu ya Tanzania Prisons kuhamia Mjini Sumbawanga, Rukwa baada ya Uongozi wa Mkoa kufanya mazungumzo na kuwasilisha kwake maombi rasmi.

Kufuatia uamuzi huo nawaomba Wananchi wa Mkoa wa Rukwa na hasa wa Mjini Sumbawanga, kujitokeza kwa wingi kuipokea timu hiyo itakapowasili rasmi hapa Sumbawanga tarehe 21 Agosti, 2020 kwa ajili ya kuweka makazi na kuanza maandalizi ya Mashindano ya Ligi Kuu ya Tanzania Bara.

Hali kadhalika nawaomba Wananchi wa Mkoa wa Rukwa kutoa Michango yao ya hali na mali ya kuiwezesha Timu hiyo kuweka Makazi yao ya kudumu hapa Sumbawanga na pia kuwezesha gharama za Maandalizi. Na ili jambo hili lifanikiwe Mkoa umeunda Kamati Maalum (Task Force) ya Watu saba (7) inayoongozwa na Mzee Chrisant Majiyatanga Mzindakaya. Wajumbe wengine ni:-

- (ii) Katibu Tawala wa Mkoa (RAS)
- (iii) Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga

- (iv) Mkuu wa Magereza Mkoa (RPO)
- (v) Mhandisi Seleman Mziray
- (vi) Patrick Mwandele
- (vii) Adam Evarist - Afisa Michezo wa Manispaa ya Sumbawanga

Michango yote ya fedha iwekwe kwenye Akaunti Namba: **9921169733** Jina La Akaunti: **RUKWA SUB TREASURY MISC. DEPOSIT EXP ACCOUNT** Benki: **BOT**

Mwisho, napenda tena kuwashukuru wadau wote waliowezesha ukarabati wa Uwanja wa Nelson Mandela na hivyo kutoa fursa ya kupata timu ya Ligi Kuu. Aidha, naomba ushirikiano endelevu utakaoiwezesha timu yetu ya Tanzania Prisons kupata ushindi.

Mungu Ibariki Tanzania

Mungu Ibariki Rukwa

Mungu Ibariki Timu ya Tanzania Prisons

Asanteni sana.